JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mtaa wa Mahakama,
S. L. P. 1419,
53103 MBEYA.
Simu: (025) 252503566
Nukushi: (025) 252502958
Barua pepe:
rbcmbeya@pccb.go.tz
Wavuti: http://www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MBEYA – 04/12/2020

TAKUKURU MKOA WA MBEYA YAFUNGUA MASHAURI MATATU (3) MAHAKAMANI NA KUSHINDA SHAURI MOJA.

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya imefungua mashauri mapya matatu Mahakamani na shauri moja lililokuwa kinaendelea Mahakamani lilitolewa hukumu ambapo ofisi yetu ilishinda.

Shauri la kwanza ni shauri la Jinai Na.272/2020 tulilofungua katika Mahakama ya Wilaya ya Mbarali (Rujewa) Dhidi ya Harrison Jordan Makinda (Hakimu Mkazi Mahakama ya Mwanzo Igurusi). Mshitakiwa anashitakiwa kwa makosa matatu ambayo ni kosa la udanganyifu na uvunjifu uaminifu kwa mtumishi wa Umma kinyume na kifungu cha 120, kutoa taarifa za uongo kwa mtumishi wa Umma kinyume na kifungu cha 122 na kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu kinyume na vifungu vya 301 na 302 vyote vya kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2002, Mshtakiwa mnamo tarehe 16/05/2019 aliwasilisha nyaraka yenye maelezo ya uongo kwa Afisa wa Gereza la Rujewa Mbarali akimtaarifu kwamba mtiwa hatiani

aliyekuwa anatumikia kifungo cha miezi 5 Jela kwakushindwa kulipa faini ya shilingi laki moja (100,000/=) na fidia ya shilingi laki sita (600,000/= baada ya hukumu, anatakiwa kutolewa gerezani kwakuwa faini ya shilingi laki moja (100,000/=) na fidia ya shilingi laki sita (600,000/= imeshalipwa. hali akijua kuwa ilikuwa ni uongo kwani kwenye hukumu aliyoiandika kwenye shauri namba 99/2019 lililokuwa linamkabili mtiwa hatiani haikuwa na adhabu ya fidia ya shilingi laki sita (600,000/=). Ingawa kiasi cha shilingi laki sita alikuwa amekichukuwa toka kwa ndugu wa mtiwa hatiani bila kupatiwa stakabadhi ya Mahakama.

Mshtakiwa alikana mashtaka na Mahakama imemwachia kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana. Shauri limepangwa kuendelea kwa hatua ya kuanza kusikilizwa upande wa Jamhuri.

Shauri la pili: Ni shauri la Jinai Na. 287/2020 tulilofungua katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Dhidi ya Gwelino Exavery Kiwoi (Mlinzi wa Kampuni ya ulinzi inayolinda majengo ya Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya). Mshtakiwa anashitakiwa kwa kosa la kupokea rushwa ya shilingi elfu arobaini (40,000/=) toka kwa mwanachuo wa chuo cha Grace kilichopo Mbeya kinyume na kifungu cha 15(1)(a) cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11/2007. Mshtakiwa alipokea kiasi hicho cha fedha baada ya kumtaka mwanachuo huyo kumpatia fedha hiyo ili amrudishie kamera na asimchukulie hatua baada ya kumkamata akipiga picha na wenzake wakiwa katika eneo la uzio wa Mahakama Kuu kanda ya Mbeya.

Mshtakiwa amekana shtaka na kupelekwa mahabusu baada ya kukosa dhamana. Shauri limepangwa kuendelea kwa hatua ya kuanza kusikilizwa upande wa Jamhuri.

Shauri la tatu ni shauri la Jinai Na. 284/2020 tulilofungua katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya dhidi ya Lilian Noel Maturo na Herieth Paul Mushi ambao ni Maafisa Wasaidizi wa Misitu Wilaya ya Mbeya. Washtakiwa wameshtakiwa kwa kosa la kupokea rushwa ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) kutoka kwa mfanyabiashara wa Mbao wilayani Mbeya aliyekwenda kufanya usajili wa biashara yake baada ya kibali alichokuwa nacho kuisha muda wake, kosa ambalo ni kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11/2007. Siku ya tukio mfanyabiashara huyo wa mbao alifika katika ofisi za wakala wa huduma za Misitu Tanzania (TFS) kufuata kibali baada ya kulipa shilingi laki mbili (200,000/=) alizotakiwa kulipa kama ada ya kufanya usajili, baada ya kufika Mshtakiwa Herieth na kumuambia kuwa hatopewa kibali mpaka atakapotoa kiasi cha shilingi elfu hamsini (50,000/=) kama faini ya kuchelewa kufanya usajili wa biashara yake alipouliza kwanini fedha hiyo haikujumuishwa kwenye bili ya awali aliyopewa kwenda kulipia, aliambiwa kuwa faini hiyo haina risiti, baada ya kupata taarifa tuliandaa mtego na kumkamata Lilian ambaye alipokea fedha hiyo siku ya tukio. Kitendo kinachoonyesha kuwa ni tabia yao na huwa wakishirikiana kufanya vitendo hivyo na ni dhahiri kuwa washitakiwa walifanya kosa hilo huku wakiwa wanajuwa kuwa kwamujibu wa sheria ya misitu kuchelewa kuhuisha kibali hakuna faini.
Washtakiwa walikana shtaka na Mahakama iliwaachia kwa dhamana baada ya kutimiza masharti. Shauri limepangwa kuendelea kwa hatua ya kuanza kusikilizwa upande wa Jamhuri.

Shauri lingine ni shauri la Jinai namba 1/2020 limetolewa hukumu katika Mahakama ya Wilaya ya Rungwe (Tukuyu) ambapo ofisi yetu imeshinda baada ya washtakiwa wote tisa (9) katika shauri hilo kutiwa hatiani. Mshtakiwa namba 1 Bw. Aladini (aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisegese katika uchaguzi wa serikali za Mitaa

uliofanyika mwezi Novemba, 2019 alishtakiwa kwa kosa la kutoa rushwa ya pombe kama kishawishi ili achaguliwe kwenye kura za maoni kinyume na kifungu cha 15(1)(b) cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11/2007. Washtakiwa wengine nane (wajumbe wa mkutano wa kura za maoni) walioshtakiwa kwa kosa la kupokea rushwa ya pombe toka kwa Bw. Aladini ili wamchague kwenye kura za maoni ili apitishwe kugombea nafasi ya mwenyekiti kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa kinyume na kifungu cha 15(1)(a) cha sheria ya kuzuia na kupamabana na rushwa namba 11/2007. Mahakama imewakuta na hatia washtakiwa wote tisa (9) na kuwahukumu kulipa faini ya Tshs, 100,000/= kila mmoja au kwenda Jela miezi 3. Washtakiwa walishindwa kulipa faini na kupelekwa Jela.

Mwisho nipende kuwapongeza wananchi wa mkoa wa Mbeya kwa kuendelea kushirikiana na Taasisi yetu katika mapambano dhidi ya rushwa. Tunawasihi kuendelea kuwasilisha taarifa za wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika ofisi zetu nasi tunaahidi kuzifanyia kazi kwa wakati.

IMETOLEWA NA:

Matechi

JULIETH MATECHI
MKUU WA TAKUKURU MKOA WA MBEYA